# Learning by Ear – Climate Change

## Episode 01

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- CAROL (14)
- LORNA (16)
- DRIVER (MALE)

Scene 2:

- JOSHUA (15)
- CAROL (14)
- LORNA (16)
- ALEX (15)
- MRS KIMAU – SCIENCE TEACHER & LORNA’S MOTHER (45)

**Intro:**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa awamu nyingine ya vipindi vya Learning By Ear “Noa Bongo Jenga Maisha yako”. Wakati huu tunaangazia mabadiliko ya hali ya hewa. Katika mfululizo wa vipindi hivi kumi vinavyofuatia, tutafuatilia maisha ya wanafunzi wane wanaosomea shule moja. Joshua mwenye umri wa miaka 15 anatoka familia maskini ya wavuvi lakini anapenda bahari. Carol ana umri wa miaka 14 na azma yake kubwa maishani ni kuwa Daktari, lakini kwa sasa huuzaji magazeti wakati wa asubuhi ili kumwezesha kulipa karo yake shuleni. Lorna naye ni msichana wa umri wa miaka 16, mwerevu, jasiri na mamake ni mwalimu wa sayansi katika shule wanakosomea. Alex ni kijana wa umri wa miaka 15 aliyekulia katika nyumba kubwa ya kifahari karibu na ufuo wa bahari. Anapata kila kitu atakacho na babake ni mbunge mashuhuri wa eneo hilo. Ingawa maisha ya wanafunzi hawa ni tofauti nyumbani kwao, shuleni wanaunganiswha na kitu kimoja – mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake maishani mwao na katika eneo wanaloishi. Hebu sasa tusikie juhudi zao za kukilinda kijiji chao na kuhifadhi mazingira zitafikia wapi. Katika kipindi hiki cha kwanza, Carol anagundua

mipango ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha umeme unaotokana na mvuke karibu na kijiji chao.

## <u>Scene One: outside in the street</u>

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **STREET/MARKET SOUNDS** |
| **1. CAROL:** | **(shouting)** Soma kila kitu…..kuhusu mradi huu mpya wa umeme! Kiwanda kipya kinaweza kuleta umeme kwa kijiji kizima! Soma kuhusu mradi huu, jipatie nakala yako ya gazeti la Dhowville Times sasa! |
| **SFX:** | **SOUND OF CAR DRIVING UP** |
| **2. DRIVER:** | Nipe nakala moja tafadhali!. |
| **3. CAROL:** | Ni senti 50 Bwana! Asante, hii hapa nakala yako!. **(shouting again)** Soma kuhusu mradi huu, mradi utakaomaliza tatizo la kukatizwa kwa umeme kijijini, nunua nakala yako sasa, soma kuhusu mradi huu. |

**4. LORNA:** Habari gani Carol, yaonekana umeuza magazeti mengi zaidi kulika ilivyo kawaida?

**5. CAROL:** Oh, Lorna, leo umerauka kwenda shuleni. Ndio, leo magazeti yamenunuliwa haraka. Nadhani ni kwa sababu ya taarifa iliyochapishwa ukurasa wa kwanza. Hebu tazama hapa kuhusu mipango ya ujenzi wa kiwanda cha umeme. **(rustle of newspaper)**

**6. LORNA:** Kiwanda kipi cha umeme, Carol?

**7. CAROL:** **K**weli mradi huu utapunguza gharama ya umeme kwa karibu kila mtu hapa kijijini - hata familia yangu pia itaweza kumudu gharama ya umeme!

**8. LORNA:** Hebu tuangalie!
**(takes paper)**

**9. LORNA:** Mmm, sina hakika kama mradi huu umenivutia! Hebu soma hapa, panasema "Kiwanda hiki kitakuwa kikubwa zaidi cha umeme unaotokana na mvuke katika eneo hili na kitalenga kutoa umeme wa bei nafuu kwa mamilioni ya watu".

**12. CAROL:** Eti unasema utakuwa mradi mkubwa zaidi katika eneo hili?

**13. LORNA:** Ndio, Carol. Na tena gazeti linasema, "kiwanda hiki kitatumia ***machujo ya petroli*** au mafuta ya ***Diesel***, aina mbili ya malighafi inayopatikana kwa urahisi". Hili linaonekena kuwa janga kubwa kwa mazingira. Hee, hii ni hatari!

**14. CAROL:** Lorna, naelewa unachosema , kweli kiwanda hiki kitakuwa tatizo kubwa kwa mazingira. Lakini machujo ya petroli na mafuta ya diseli yana ubaya gani?

**15. LORNA:** Unajua, mafuta mazito yanayobakia baada ya petroli kusafishwa ili kutoa mafuta ya diesel, mafuta ya taa hayafai. Ni mazito mno na huwa yamejaa taka!

**16. CAROL:** Mabaki haya ya mafuta hufanywa nini?

**17. LORNA:** Ahh, nimesoma kuwa meli nyingi hutumia mafuta haya kwa sababu ni nafuu. Na pia nasikia kuwa hutoa gesi ya sumu wakati yanapochomwa. Kwa hiyo nadhani yatatumiwa kutoa umeme kwa ajili ya kiwanda hiki. Hebu fikiria, hewa ya sumu kutoka kiwandani tutakayolazimika sote kupumua.

**18. CAROL:** Nafahamu unachosema. Mabaki ya mafuta, yuuuk!, na kama kiwanda hiki ndicho kitakachokuwa kikubwa zaidi katika eneo hili, hebu fikiria kiasi cha machujo ya mafuta yatakayotumika. Maelfu na maelfu ya tani…!

**19. LORNA:** Carol, hebu tazama ukurasa wa pili wa gazeti, "Wataalam wa mazingira waonya kiwanda kipya cha umeme kitachangia pakubwa mabadililiko ya hali ya hewa yanayotokana na gesi za viwandani."

**20. CAROL:** Mmm, Nashangaa hiyo ina maana gani….

**21. LORNA:** Makala inaendelea, "gesi zitakazototolewa kutoka kiwanda hicho huenda zikasababisha hali mbaya zaidi ya hewa katika eneo hili na kusababisha mafuriko na hata ukame. Carol, kila kitu kinakanganya kidogo, ama sivyo?

**22. CAROL:** Lorna, Nadhani tutajifunza mengi zaidi katika darasa letu la Sayansi..

**23. LORNA:** Kweli,…vyovyote vile.. sasa tunapaswa kwenda shuleni haraka la sivyo tutachelewa. Nikusaidie kufunga kibanda?

**24. CAROL:** Kwani tayari saa zimefika? Sawa, litakuwa jambo zuri ukinisaidia. **(Sound of moving papers)**

**Scene Two: classroom**

**SFX ATMO:** **SCRAPING CHAIRS & DESKS**

**25a. All:** **(Chatter).**

**25b. JOSHUA:** Hujambo Lorna, nafurahi kwamba mama yako ni mwalimu wetu wa Sayansi mwaka huu. Anaonekana kazi yake.

**26. LORNA:** Asante sana kwa kunihifadhia nafasi ya kuketi Josh! Ni Kweli mamangu, anapenda sana kufunza sayansi, hasa kuhusu masuala yote ya mazingira. Nadhani anahisi inatufaa kwa kuwa sisi tunaoishi Afrika ndio tunaoathiriwa zaidi wakati majanga asili yanapotokea.

**27. JOSHUA:** Mmm, hiyo ni kweli. Habari Alex, umekamilisha kazi yako ya shuleni? Leo ni siku yetu sisi wawili kutoa mhadhara kuhusu athari za gesi za viwandani. Je umefanya utafiti wako?

**28. ALEX:** **(pulling up a chair)**
Nilijaribu kusoma kidogo kuhusu swala hili, lakini kusema kweli, naliona linachosha. Ohh ***Greenhouse*** hivi…..! ohh ***greenhouse*** vile! Hata hivyo babangu anasema huo ni upuuzi mtupu..

**SFX:** **OPENING OF A DOOR, FOOTSTEPS**

**31. MRS KIMAU:** Habari za asubuhi. Leo tunajifunza mada muhimu sana. Athari za gesi za viwandani, na Alex na Joshua watatupa utangulizi mfupi wa mada hii. Alex?….Joshua?

**32. JOSHUA**: Ndio Bi Kamau. Nafikiri nitaanza kisha Alex ataongezea maoni zaidi, ama sivyo Alex?

**33. ALEX:** Mmm, sawa.

**34. JOSHUA:** Aaah, basi nadhani nitaanza kwa michoro, kufafanua suala lenyewe.

**SFX:** **SOUND OF CHALK ON BLACKBOARD**

Na kitu cha kwanza kuchora ni nyumba ya kioo kama ile inayotumiwa na wakulima wa maua kama mashamba ya kukuza maua yao.

**SFX:** **SOUND OF CHALK ON BLACKBOARD**

Unapoingia katika nyumba hii ya kioo hasa kunapokuwa na jua kali, inakuwaje?

**35. ALEX** Aaah, bila shaka huwa na joto kali!

**36. JOSHUA** Hasa…! Hii ni kwa sababu kioo kilichotumika kujenga nyumba hii ya kukuza maua, hunasa joto kutoka kwa miale ya jua. Na kadhalika kuna aina fulani ya gesi zinazofanya vivyo hivyo katika anga yetu...

**37. MRS KIMAU**: Je unaweza kunitajia gesi yoyote inayochafua mazingira?

**38. JOSHUA:** Ehh ndio…mfano mzuri ni dioksidi ya Kaboni. Lakini hata mvuke wa maji pia. Vyote hivi vina athari sawa katika angahewa ya ardhi!

**39. ALEX** Kivipi?

**40. JOSHUA:** Ehh, kioo cha nyumba ya kioo huifanya mimea au maua kuwa vuguvugu, si ndio?

**41. ALEX:** Sawa kabisa!

**42. JOSHUA:** Na kwa njia hiyo hiyo gesi hizo za viwandani huifanya ardhi kuwa vuguvugu. Bila ya hivyo, tungekuwa tunakufa kwa baridi kali. Lakini joto likizidi in amaana tutakuchemka kama maji.

**43. MRS KIMAU:** Joshua na Alex, kwa nini mnafikiri athari za majumba haya ni tatizo kubwa kwetu siku hizi?

**44. JOSHUA:** Aaah, siku hizi tunatumia nishati zaidi kuliko zamani zenye kaboni kama vile mafuta, gesi na makaa ya mawe, kuendesha magari yetu na kutoa umeme kwa ajili ya vivanda vyetu.

**45. MRS KIMAU:** Hasa.

**46. JOSHUA** Vyote hivi hutoa gesi chafu kama vile dioksidi ya Kaboni.

**47. ALEX:** **(almost thinking/speaking out loud)**
Ahhh kumbe..! na kisha kiwango cha joto kinaongezeka katika sayari yetu. Wau, inaeleweka!

**48. MRS KIMAU:** Hivyo ndivyo wanasayansi wengi wanavyofikiria Alex! Na ndio sababu athari za gesi za viwandani ni tatizo linalozua wasiwasi mkubwa kwa sisi hapa Dhowville, na kwa dunia nzima! Hofu iliyopo ni kwamba kadri dunia inavyoendelea, ndivyo tutakavyohitaji umeme zaidi na kupeleka magari zaidi na hiyo ina maana kujiweka katika hatari ya kutoa gesi zaidi zinazoathiri mazingira.

**51. CAROL:** Umesema athari hizi hutokea tunapotumia umeme? Kwa sababu nimesoma tu leo katika gazeti kwamba kuna mipango ya kujenga kiwanda cha umeme hapa hapa Dhowville.

**52. MRS KIMAU** Aaah, hapana, lakini inategemea jinsi umeme huo unavyotengenezwa. Tunahitaji kuchunguza ikiwa kiwanda hicho kitachafua mazingira au kitakuwa chanzo safi cha umeme.

| | |
|---|---|
| **53. CAROL:** | Aaah sawa, Bi Kamau, ninahakika nimesoma kwamba kiwanda hicho kitatumia machujo ya mafuta ya petroli au diesel. Tumesoma katika gazeti la leo. |
| **55. MRS KIMAU:** | Sawa, Carol, hilo halisikiki kuwa jambo la kutia wasiwasi. Tutalizungumzia zaidi kwa kina hapo kesho! |
| **SFX:** | **SOUND OF LESSON BELL** |
| **SFX:** | **SCRAPING OF CHAIRS** |
| **56. ALEX:** | **(talking to Joshua)**<br>Oh, Najua. Babangu amekuwa akikizungumza sana kiwanda hiki. Anadhani ni wazo zuri la kushangaza litakalokuwa na manufaa makubwa kwetu! |

**57. JOSHUA:** Nina hakika familia nyingi ma marafiki hawana habari kuhusu athari zinazotokana na gesi zinazochafua mazingira na ongezeko la ujoto duniani. Unapaswa uzungumze naye, Alex. Tuonane kesho!

**END OF EPISODE ONE**

**Outro:**

Na hadi hapo ndipo tunafika mwisho wa kipindi cha leo. Mchezo kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ulioandikwa na Victoria Averill. Ungana nasi wakati mwengine usikie jinsi Alex atakavyotofautiana na Babake kuhusu mpango wa ujenzi wa kiwanda kipya cha umeme kijijini mwao. Pia utasikia jinsi Alex, Lorna, Carol na Joshua wanavyopanga kupinga mradi huu. Usikilize tena mchezo huu, tembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe
Hadi wakati huo kwaheri kwa sasa.